

Maswali

1. Eliya alimtumia Ahabu habari gani?
2. Ahabu aliabudu Mungu gani
3. Eliya aliwaagiza wafanye nini?
4. Manabii wa Baali walikuwa wangapi?
5. Ni jaribio gani aliwawekea?
6. Manabii wa Baali walicheza kwa mda gani?
7. Baali alipata jibu gani?
8. Eliya alifanyaje dhabihu yake?
9. Eliya alipata jibu gani?
10. Watu walisema nini?
11. Eliya aliamrisha nini?
12. Wingu ndogo ilimaanisha nini?

Majibu

1. Mvua itanyesha tena
2. Baali
3. Waitishe mkutano mkubwa kwa mlima wa Karmeli.
4. 450
5. Mungu anayejibu kwa moto ndiye Mungu
6. Siku mzima
7. Hakupata jibu
8. Aliimwagia maji
9. Moto kutoka mbinguni
10. Bwana ndiye Mungu
11. Wawauwe manabii wa Baali wote.
12. Kutakuwa na mvua nyingi

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 1

28 Eliya kwa mlima wa Karmeli

Marejeo

1 Wafalme 18:1—40

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu ni Mungu yeye wa kweli pekee

Maneno maalum

1. Kiangazi + miaka 3 + tuma Eliya + mvua tena.
2. Ahabu + Baali + kasirisha Mungu + hakuna nguvu.
3. Mkutano mkubwa + manabii 450 + Karmeli + Israeli yote.
4. Chagua + jaribu + dhabihu + bila moto + piga kelele + hakuna jibu.
5. Jioni + dhabihu + maji + maombi + moto kutoka binguni.
6. Ua manabii + wacha kuabudu Baali.
7. Bahari + wingu + mara 7 + mvua+ Mungu abariki.

28.1 Hakukuwa na mvua Israeli na kila pahali kukakauka. Mwishowe Mungu alituma Eliya amwambie Ahabu kwamba kutakuwa na mvua tena. Kabla ya mvua Mungu alitaka Ahabu na Waisraeli wote wajue kwamba, Mungu ni wa kweli na mwaminifu.

28.2 Ahabu na watu wote hawakukuwa wakiabudu Mungu wa kweli kamwe. Waliabudu mungu wa uongo aliyeitwa Baali. Hii ilimkasirisha Mungu, kwanza akazuia mvua, hivyo awaonyeshe kwamba Baali hana nguvu na hangewafanyia chochote.


28.3 Eliya alimwambia Ahabu awaite watu wengi. Manabii 450 wa Baali walitakiwa waende kwa mlima wa Karmeli ulioko Israeli. Mlima ulikuwa karibu na bahari. Watu wa Israeli nao wakitwa kuenda kwa huo mkutano. Mkusanyiko ulikuwa mkubwa muno.

28.4 Eliya aliwauliza wachague Mungu wa kweli, akafanya jaribio waone kama Baali anafaa kuliko Mungu wa Israeli. Waliangalia na kusikiliza kwa utulivu, jaribio lilikuwa hivi. Manabii wa Baali wafanye dhabihu kwa kuweka fahali juu ya kuni na wasiweke moto kwa kuni.

Badala yake waite Baali ajibu kwa kulete moto. Manabii wakafanya hivyo.

Wakacheza.
Wakaimba.
Wakapiga kelele.

Asubuhi yote waliendelea. Eliya aliwambia wapige kelele zaidi, waliita zaid kwa siku nzima mpaka jioni hakukuwa na jibu.



28.5 Ilipofika jioni alituliza watu na kuweka fahali ya dhabihu juu ya kuni. Aliambia watu wamwage maji juu ya kuni mara tatu, akaomba Mungu. Maombi yake ilikuwa kwa Mungu wa Ibrahimu, Isaka na Yakobo. Alitaka watu waelewe na wajue Mungu wa Israeli ndiye wa kweli.



Papo hapo moto ulishuka kutoka mbinguni na kuchoma dhabihu pamoja na kuni, na tena ulikausha maji. Watu walishangaa na kusema, “Bwana ndiye Mungu! Bwana ndiye Mungu!”

28.6 Eliya alipinduka na kuamrisha watu wawaue manabii 450 wa Baali. Walikuwa wameona nguvu za Mungu wa Eliya lakini hawakuona chochote kwa Baali. Walikubali na siku hiyo waligoma kuabudu Baali katika Israeli.

28.7 Baadaye Eliya aliuliza mtumishi wake angalie juu ya bahari na hakukuwa na kitu. Alimtuma mara nyingi akienda, mwishowe, mara ya saba, mtumishi alimwambia ameona wingu ndogo. Eliya aliwambia wajitayarishie mvua nyingi. Mwisho wa kiangazi ulikuwa umewadia(umefika). Mungu alikuwa tayari kubariki watu wake tena kwa sababu walimtambua yeye kama Mungu wa kweli.